



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA MBULU



Unapojibu tafadhali taja:

22 Machi, 2022

TANGAZO LA KUITWA KWENYE USAILI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu anawatangazia wote waliomba kazi ya **KARANI WA KUSAJILI ANWANI ZA MAKAZI** kufika kwenye usaili utakaondeshwa tarehe **25 Machi, 2022** kuanzia saa **9:00** kamili asubuhi kulingana na vituo vilivyopangwa kama ifuatavyo:-

a. Kanda ya Dongobesh

Mahali: Shule ya Sekondari Dongobesh

Waombaji kutoka kata za Dongobesh, Tumati, Yaeda Ampa, Gidhimu, Dinamu, Bashay na Maretadu.

b. Kanda ya Haydom

Mahali: Shule ya Sekondari Dr. Olsen

Waombaji kutoka kata za Haydom, Geterer, Hayderer, Endamilay, Yaeda Chini, Eshkesh, Maghang na Labay

c. Kanda ya Mbulu Mjini

Mahali: Ukumbi wa Chama Cha Walimu Tanzania (CWT)

Waombaji kutoka kata za Masqaroda, Endahagichan na Masieda

Wasailiwa wanaoitwa kwenye usaili wanapaswa kuzingatia maelekezo yafuatayo:-

- I. Kufika na Simu **JANJA**
- II. Kila Msailiwa anapaswa kuwa na kitambulisho kwa ajili ya utambuzi;
- III. Vitambulisho vinavyokubalika ni pamoja na:- Kitambulisho cha Mkazi, Kitambulisho cha Mpiga kura, Kitambulisho cha kazi, Kitambulisho cha Uraia au Hati ya kusafiria;
- IV. Wasailiwa wanatakiwa kufika na **VYETI VYAO HALISI**, kuanzia cheti cha kuzaliwa, kidato cha IV, VI, Astashahada kutegemeana na sifa za Mwombaji;
- V. Wasailiwa watakaowasilisha "Testimonials", "Provisional Results", "Statement of results", hati za matokeo za kidato cha IV na VI (form V and form VI results slips) **HAVITAKUBALIWA NA HAWATARUHUSIWA KUENDELEA NA USAILI;**
- VI. Kila msailiwa atajigharamia kwa Chakula, Usafiri na Malazi;
- VII. Kila Msailiwa azingatie tarehe, muda na mahali alipopangiwa kufanyia usaili;
- VIII. Kwa waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe Vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (kama TCU, NACTE au NECTA);

IX. Waombaji kazi ambao majina yao hayakuonekana katika tangazo hili watambue kuwa hawakukidhi vigezo. Hivyo, wasisite kuomba tena pindi nafasi za kazi zitakapotangazwa na kuzingatia mahitaji ya tangazo husika;

MAJINA YA WANAOTWA KWENYE USAILI IMEAMBATANISHWA HAPO CHINI: -

Tangazo hili pia linapatikana kupitia tovuti ya Halmashauri www.mbuludc.go.tz na mbao za **Matangazo**

Imetolewa na;

Protas Sulle
KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA YA MBULU.